Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

25/= Ksh

Volume 3, Issue 1
22nd Shawwal 1431
1st October, 2010

Yaliyomo

Kujenga Undugu 1– 3
Damu Asilia za wanawake 3 - 4

KUJENGA UNDUGU

Mtayarishi: Imaam, Al-Haafidh Ibn Abee Ad-Dun'yaa (رحمه الله) [F. 281H]

Mlango: Kuwahusu Wale Wenye Kupendana Kwa Ajili Ya Allaah, Na Fadhla Zao Mbele Ya Allaah

Amepokea al-Baraa' Bin 'Aazib (رضي الله عنه) "Nilikuwa nimekaa mbele ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliposema: '*Munajua ni mashiko gani ya Imaan yaliyo na nguvu zaidi?*' Tukasema: 'Ni swala.' Akasema (صلى الله عليه وسلم) '*Swala ni nzuri, lakini hiyo siyo.*' Kisha akataja baadhi ya Sheriya za Uislamu na alipoona yakwamba hatulipati suala lake vyema, akasema (صلى الله عليه وسلم) '*Mashiko ya Imaan yaliyo na nguvu zaidi ni kwamba unapenda kwa ajili ya Allaah na kuchukuia kwa ajili ya Allaah* (عزّ وجلّ)".

Al-'Irbaadh Bin Saariyah (رضي الله عنه) amepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Amesema Allaah* (تبارك وتعالى), '*Wenye kupendana kwa ajili ya Utukufu wangu watakuwa chini ya kivuli cha 'Arshi yangu katika siku ambayo hapatokuwa na kivuli isipokuwa kivuli changu.*'"

Amepokea Abu Hurairah (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: " *Allaah* (تبارك وتعالى) *atasema: 'Wako wapi wale wenye kupendana kwa ajili ya Utukufu wangu? Leo, nitawakinga na kivuli Changu, kwenye siku ambayo hapatokuwa na kivuli isipokuwa kivuli Changu.*'"

Amepokea Abu Hurairah (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Kwa hakika, miongoni mwa waja wa Allaah, ni waja (fulani) ambao watakao onewa wivu na Mitume na Mashahidi.*" Wakasema (Maswahaba – kumwambia Mtume (صلى الله عليه وسلم) "Ni kina nani hao, ili nasi tuwapende?" Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم) "*Hao ni kundi la watu wenye kupendana kwa ridhaa ya Allaah, si kwa ajili ya mali wala nasaba. Nyuso zao ni miangaza. Watakuwa juu ya majukwaa ya miangaza. Hawana khofu pindi watu wanapokuwa na khofu na wala hawahuzuniki pindi watu wanapohuzunika.*" Kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawasomea: "*Hapana shaka! Kwa hakika, ma-Awliyaa' (mawalii wa Allaah), hawatopata khofu yoyote, wala hawatohuzunika.*".

'Amr Bin 'Abasah amehadithia yakwamba amemsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema: "*Kwa hakika, Allaah amesema: 'Mapenzi yangu yanawajibika juu ya wale wenye kupendana kwa ajili Yangu. Na mapenzi yangu yanakuwa ni haki juu ya wale wenye kufanya urafiki kwa ajili yangu.*'"

Amesema 'Ubaadah Bin as-Saamit (رضي الله عنه) "Nilimsikiya Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وسلم) akipokea kutoka kwa Mola wake (تبارك وتعالى) yakwamba alisema: '*Mepenzi yangu yanakuwa ni haki juu ya wenye kupendana.Watakuwa kwenye kivuli cha 'Arshi siku ya Qiyaamah, ambapo hapatokuwa na kivuli isipokuwa kivuli Changu.*'"

Amepokea Abu Sa'eed (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Hakika, ni wa Allaah* (عزّ وجلّ) *waja ambao watakaokuwa juu ya majukwaa yenye muangaza chini ya kivuli cha 'Arshi siku ya Qiyaamah. Na Mitume na Mashahidi watawaonea wivu. Nao ni wale wenye kupendana kwa ajili ya Allaah* (عزّ وجلّ)."

Ibn Fudhayl amepokea yakwamba babake amesema: "Nilikutana na Abu Is-haaq baada ya kupoteza macho yake (yaani; alikuwa kipofu). Alinishika mkono, nami nikamwambia: 'Ushanitambua mimi?' akajibu, 'Ndio, naapa kwa Allaah yakwamba nimekutambua, na kwa hakika mimi nakupenda. Na lau kama si kuona haya, basi ningelikubusu. Wewe wajua Aya hii iliteremshwa kwa ajili ya nani? Abu al-Ahwas amenihadithia yakwamba 'Abdullaah (رضي الله عنه) amesema (Imeteremshwa) kwa wenye kupendana kwa (ajili ya) Allaah: **'Na aliziunganisha nyoyo zao (kwa mapenzi), lau ungetumia yaliyomo ardhini yote hungeweza kuwaunga nyoyo zao lakini Allaah aliwaunganisha baina yao.'** [al-Anfaal 8:63]

Abu Umaamah (رضي الله عنه) amesema, [amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم) "*Yoyote mwenye kupenda kwa ajili ya Allaah na kuchukia kwa ajili ya Allaah, na kutoa kwa ajili ya Allaah na kuzuiya*

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

KUJENGA UNDUGU

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

kwa ajili ya Allaah, basi itakuwa Imaan yake imekamilika."

Abu Umaamah (رضي الله عنه) amesema, amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم) *"Hapana mja mwenye kumpenda mwenziwe, isipokuwa Allaah humkirimu (humfadhili)."*

Mlango: Kuwahusu Wale Ambao Tuloamrishwa Kuwa Nao Na Ushawishi Wenye Kupelekea Kuthibitisha Mapenzi Juu Yao

Amepokea Abu Hurairah (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Mtu huwa juu ya dini ya rafiki yake wa karibu. Basi kila mmoja wenu na aangalie kwa umakini ni yupi anaemfanya kuwa rafiki wa karibu."*

Amepokea Abu Sa'eed (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Usimfanye (yoyote) kuwa ni rafiki yako isipokuwa mu'min. Na wala usimuache yoyote kula katika chakula chako isipokuwa mtu aliye na Taqwaa (anaemcha Allaah)."*

Maalik Bin Maghool amepokea yakwamba al-Hasan amesema: "Baadhi ya watu waliuliza; 'Ewe Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وسلم) ni Maswahaba gani walio bora?' Akajibu Mtume (صلى الله عليه وسلم) *"Ni Swahaba ambaye unapomtaja Allaah* (تبارك وتعالى) yeye hukusaidia. Na unapomsahau (Allaah), yeye hukukumbusha". Wakasema, 'Ewe Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وسلم) Tuelekeze nasi kwa aliye mbora wao kutoka miongoni mwetu ili tuwafanye kuwa ni rafiki zetu.' Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم) *Ndio, ni wale ambao pindi wanapoonekana, Allaah hukumbukwa.'*

Furaat Bin Salmaan amepokea yakwamba al-Hasan amesema: "Mu'min ni kioo kwa ndugu yake. Anapoona jambo kwake asilolipenda, hulionyesha, akalirekebisha, akalificha na akalilinda penye kufichika na penye kudhihirika. Kwa hakika, kwenye rafiki yako wa karibu ni fungu lako na kwa hakika kwako wewe ni fungu kutokana na kumtaja umpendaye. Kwahiyo, chagua marafiki waaminifu, ndugu, na unaokaa nao."

Mlango: Matangazo Ya Mtu Kwa Nduguye, Bila Ya Utani Kuhusu Jinsi Anavyompenda

Amepokea Al-Miqdaad Bin Ma'dee Kurb (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Anapompenda mmoja wenu nduguye na ampashe khabari yakwamba anampenda."*

'Uthmaan Bin al-Aswad amepokea yakwamba Mujaahid amesema: "Ni haki juu ya mtu, pindi anapompenda nduguye kwa ajili ya Allaah yakwamba na amjuze."

Zubeyd amepokea yakwamba Mujaahid amesema: "Imehadithiwa kwangu yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Atakapompenda mmoja wenu nduguye kwa ajili ya Allaah, basi na amjuze (kuhusu jambo hilo). Kwani kwa hakika, linabaki hilo katika udugu na huongeza nguvu katika kupendana."*

Habeeb Bin Dhabee'atu adh-Dhab'ee (رضي الله عنه) amesema: "Mtu mmoja alikuja kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), mara mmojawapo wa Maswahaba wake akasema: 'Hakika mimi nampenda huyu kwa ajili ya Allaah.' Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: *"Ushamwambia (kuhusu jambo hilo)."* Akajibu: 'Laa.' Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: *"Basi simama na umjulishe."* Kwahivyo akamsimamia na akamwambia: 'Ewe fulani, kwa hakika mimi nakupenda kwa ajili ya Allaah!' Nae akamjibu: "Namuomba yule ambaye kwa ajili yake unanipenda, Nae Akupende."

Thaabit amepokea yakwamba Anas Bin Maalik (رضي الله عنه) amesema: "Siku moja, mtu mmoja alikuwa amekaa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) mara akapita mtu mwengine. Basi yule mtu [aliyekuwa amekaa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: 'Ewe Mjumbe wa Allaah, kwa hakika mimi nampenda yule.' Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: *"Basi mjuze kuhusu ukweli huo, kwani kwa hakika hiyo ndiyo njia bora ya kuyathibitisha mapenzi baina yenu nyinyi wawili."*

Mlango: Kufanyiana Ziyara Baina Ya Ndugu

Amepokea Abu Hurairah (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Palikuwa na mtu mmoja aliyetoka na kwenda kumzuru nduguye kwenye kitongoji (tafauti), basi Allaah akamuekea Malaika awe ni mwenye kumungoja kwenye barabara. Akasema (Malaika) kumwambia yule mtu: "Kwani wewe wendapi?" Akajibu: 'Mimi nenda kumzuru ndugu yangu kwenye kijiji hiki.' Akasema: "Kwani wewe ulimfanyia kitu ambacho unahitaji malipo?' Akasema: 'Laa, mimi nampenda tu kwa ajili ya Allaah." Malaika akamwambia: "Basi kwa hakika mimi ni mjumbe kutoka kwa Allaah, niliyetumilizwa kwako (kukupasha khabari) yakwamba Allaah* (عزّ وجلّ) anakupenda kama ambavyo wewe ulivyompenda."

'Ubaadah Bin as-Saamit amepokea yakwamba alimsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisimulia kutoka kwa Mola wake yakwamba alisema: *"Mapenzi yangu yanakuwa ni haki kwa wenye kutembeleana kwa ajili Yangu."*

Amesema Abu Umaamah (رضي الله عنه) "Miongoni mwa yenye kutimiza maamkuzi yenu ni kupeana mikono."

Amepokea Qays yakwamba Jareer (رضي الله عنه) amesema: "Tangu niliposilimu, Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwahi kuniona mimi isipokuwa kwa uso mteshiteshi."

Mlango: Kuhusu Kuwalisha

(Endelea kwenye Ukurasa wa 3)

KUJENGA UNDUGU

[...Damu Asilia]

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

Chakula Ndugu Zako, Fadhla Zake Na Kutilia Mkazo Kuyafanya Hayo

Amepokea 'Ataa' yakwamba 'Abdullaah Bin 'Amr (رضي الله عنه) amesema [kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema]: *"Chakula chenye kupendekeza mno kwa Allaah (عزّ وجل) ni kile chenye kuingia juu yake mikono mengi."*

Ni Nani Ibn Abee Ad-Dun'yaa (رحمه الله) [F. 281h]

Yeye ndiye aliyeandika Kitabu hiki. Nae ni 'Abdullaah Bin Muhammad Bin 'Ubayd al-Baghdaadee al-Hanbalee, maarufu kwa jina Ibn Abee ad-Dun'yaa (رحمه الله) Alizaliwa Mjini Baghdaad katika mwaka wa 208 H wakati wa khilaafah ya Ma'moom. Alizaliwa kutoka kwenye jamii nzuri iliyosifika kwa 'ilmu. Babake alikuwa ni mmojawapo wa wanavyuoni wa sehemu aliyokuwa akiishi, na kwa ajili hiyo, alikuwa akimchukuwa na akikaa nae na baadhi ya wanavyuoni wakubwa na *mahuffaadh* (wingi wa *haafidh*) wa zama hizo. Kwahiyo, kuanzia kwenye umri mdogo, al-Haafidh (رحمه الله) alikuwa akilelewa juu ya 'ilmu. Mashekhe (waalimu) wake ambao aliowahi kusikiya na kupokea hadeeth kutoka kwao, wamefikiya idadi kubwa sana. Imaam adh-Dhahabee (رحمه الله) aliwahesabu na kufikiya Tisaini na Nne (94) [Angalia kwenye *Siyaar A'laam an-Nubalaa'* 13/397]. Katika mojawapo ya vitabu vyake, "*Sifat ul-Jannah*" (Jinsi ilivyo Pepo). Al-Haafidh (رحمه الله) amepokea kutoka kwa wapokezi zaidi ya Mashekhe Mia Mbili (200); Kwahiyo malezi aliyokulia na kutafuta kwake 'ilmu yalikuwa ni makubwa mno. Alikuwa ni mmojawapo wa wanavyuoni wa hadeeth waliotegemewa wakati wa zama zake. Aliwahi kuwafunza watoto wa ma-khaleefah, jambo ambalo lililoshaji'isha mujatama' wake. Wanafunzi walikuwa wakisafiri kutoka sehemu mbalimbali ili wapate kumsikiya na kufaidika kutoka kwake. Kwa sababu hii, Imaam Ibn Abee ad-Dun'yaa (رحمه الله) alipata mojawapo ya *ta'dhima* kubwa katika Uislamu kuhusiana na 'ilmu ya hadeeth. Vitabu vyake vimefikia kwenye mamia kwenye mas'ala mbalimbali. Ibn Katheer (رحمه الله) amesema kumuhusu yeye: "Alikuwa ni *Haafidh* (kwenye hadeeth), mtungaji maarufu wa vitabu chungu nzima vyenye manufaa." Adh-Dhahabee amesema kumuhusu yeye: "Alikuwa ni *Muhaddeeth* (mwanachuoni wa hadeeth), mwanachuoni na mtu muaminifu wa kutegemewa." Ibn al-Jawzee (رحمه الله) amesema yakwamba yeye alikuwa ni mwenye kutokamana na wenye kutegemewa waliokuwa na uaminifu. Na hali yake ya ustahilifu inaendelea hivyo. Alikufa katika siku ya Jumanne, usiku wa tarehe ya Kumi na Nne, Jumaadee al-Aakhira, mwaka wa 281H. Twamuomba Allaah Amrehemu na amja'alie daraja ya Juu Peponi – Aameen.

Makala haya yana ahaadeeth zilizochaguliwa kutoka kwenye kitabu cha Sheikh *"Kitaab ul-Ikhwaan"* (Kitabu Cha Undugu). Usahihishaji wa ahaadeeth umefanywa na Ahmad 'Abdur-Rahmaan at-Tawaalibah na marejeo ya kumbukumbu yamefanywa na Dr. Najm 'Abdur-Rahmaan Khalaf wa Egypt.

Al-Rahma 'Umrah & Hajj Agencies. Twawatangazia Mpango wa Safari ya Hajj ya Mwaka huu 1431H/2010 C.E

Tutakwenda na wewe mguu kwa mguu tuitekeleze 'amali hii pamoja Insha-Allaah. Twakuhakikishia Uaminifu wetu. Njoo utuone kwenye Ofisi yetu, Mombasa.

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 4)

baadae, hapo kutakuwa kumeingia mas'ala ya urathi baina yao. Kujua iwapo mwanamke anayo mimba au hana mimba, kunathibitisha hali ya ugawanyaji wa urathi. Huyu mume aliyemuowa hatoruhusiwa kuingiliana nae mpaka baada ya Kupata damu ya heidh, kuashiriya yakwamba fuko lake la uzazi halina mimba na kwahiyo hakuna mas'ala ya urathi. Mimba yake wakati alipokufa mwenye kurithiwa imethibitishwa waziwazi. Katika hali hii, ugawanyaji wa urathi ni lazima umzingatie yule mzaliwa mpya.

Ya Kumi: Uwajibu Wa Kujitwahirisha (Ghusl)

Ni waajib juu ya mwanamke mwenye heidh aoge pindi amalizapo heidh yake. Hii ni kulingana na maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipomwambia Faatimah (bintiye Abee Hubaish): *"Ukipata ada yako ya mwezi, wacha kuswali, na ikiwa imekwisha, jitwahirishe kwa kuoga na utekeleze swala."* [al-Bukhaari]

La kufanya kwa uchache katika kuoga (kujitwahirisha), ni kueneza maji juu ya kiwiliwili chote ikiwemo ngozi ya kichwa na nywele zake. Njia bora ya kuoga ni ile iliyofundishwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) wakati Asmaa', bintiye Shakl alipouliziya kuhusu "Ghusl"na Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: *"Kila mmoja wenu na atumie maji (yaliyochanganywa na majani ya) mti wa lote na ajisafishe nayo kwa kujisugua, kisha na ajimwagie maji juu ya kichwa chake na ajisugue mpaka aguse mizizi ya nywele zake. Kisha na ajimwagie maji juu yake. Baada ya hapo achukuwe kipande cha pamba kilichonyunyiziwa misk na akitumie kujisafishe nacho."* Asmaa akasema, "Atajisafisha nacho vipi?"Kufikia hapo, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamaka, *"Subhaanallaah! Atajisafisha nacho."* 'Aaisha (رضي الله عنهما) akasema (kwa sauti ya chini) yakwamba atajisafisha kwenye alama za damu. Mwanamke mwenye heidh hawajibiki kuzifungua nywele zake anapokuwa tayari kutekeleza Ghusl (kuoga), isipokuwa ikiwa nywele zake zimekazwa mno kiasi cha kwamba zitazuiya maji yasipenye na kufika chini ya nywele.

[Endelea katika Makala Yajayo]

Ukumbi Wa Wanawake

... Damu Asilia Za Kina Mama [Sheikh Muhammad bin Swaleh al-'Uthaymeen (رحمه الله)

(Endelea kutoka Vol 2, Issue 2)

"Ewe Mjumbe wa Allaah! Mimi simlaumu Thaabit kwa kasoro katika tabia yake wala dini yake, lakini mimi kama Muislamu, sipendi kuwa katika tabia isiyokuwa ya ki-Islamu (iwapo nitaendelea kuwa nae)". Juu ya hayo Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: *"Utamrudishia mumeo shamba lake alilokupa (kama Mahr)?"* Akasema: "Ndio." Kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia Thaabit: *"Ewe Thaabit! Chukuwa shamba lako, na umuache talaka moja."* Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuuliza iwapo mkewe Thaabit alikuwa kwenye heidh au laa. Chini ya hali kama hizi za mahitaji ya kikweli, mke anaweza kuomba talaka yake bila ya kujali kuhusu hali ya ada yake ya mwezi. "Kumpa talaka mwanamke wakati akiwa kwenye heidh huwenda kukamdhuru mwanamke kwa sababu kutarefusha Eda yake. Na kwa upande mwengine, madhara yanayopatikana kutokana na mateso na ugomvi mkubwa ni makubwa zaidi kuliko pigo la madhara yaliyotokamana na urefushaji wa Eda, na kwahivyo ni muhimu zaidi kuiondoa dhiki hiyo kwa njia ya kutala talaka. Hii ndiyo sababu kwa nini Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuuliza kuhusu hali ya heidh ya mkewe Thaabit Ibn Qays."

Mas'ala: Kuithibitisha ndoa na mwanamke aliye kwenye heidh inaruhusiwa kwa sababu hakuna dalili inayoashiriya kinyume chake. Hatahivyo, mume na atahadharishwe yakwamba iwapo hatoweza kujizuiya na uchu wake, basi na asikae faragha na mkewe mpaka atwahirike kutokamana na heidh yake.

Ya Nane: Heidh na Eda ya Talaka.

Iwapo mume amemuacha mkewe baada ya kumuingilia kwa mara ya kwanza au baada ya kuwa nae faragha, basi itampasa akae *Eda kwa muda wa mihula mitatu* (ikiwa atakuwa ni mwanamke mwenye heidh na wala sio mwenye mimba). Hii ni kulingana na maneno ya Allaah (سبحانه وتعالى) **"Na wanawake walioachwa wangoje (wasiolewe) mpaka twahara tatu zishe."** (Al-Baqarah 2:228)

Ikiwa atakuwa ana mimba basi Eda yake ni mpaka atakapozaa (kwa muda wowote wa mimba utakaokuwa, mrefu au mfupi), kwa sababu amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na wanawake wenye mimba eda yao ni mpaka watakapozaa."** (at-Talaaq 65:4)

Hatahivyo, ikiwa mwanamke ni miongoni mwa wale wasopata heidh kama msichana mdogo ambae hajafika umri wa kupata heidh au ambae ashapita umri wa ada ya kila mwezi au alifanyiwa upasuaji na kutolewa fuko la uzazi, na kadhaalika; basi Eda yake ni miezi mitatu kutokana na maneno ya Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na wale waliokoma na kutoka heidh miongoni mwa wanawake wenu, ikiwa mnayo shaka (katika muda wao wa Eda), basi muda wa Eda yao ni miezi mitatu, na (pia ndiyo Eda kwa wale) ambao hawajapata heidh bado."** (At-Talaaq 65:4) [Isipokuwa iwapo ni mas'ala ya kifo (Tizama katika Qur'an 2:234)]

Mas'ala: Tuseme mwanamke alikuwa ni miongoni mwa wale wenye kupata ada zao za kila mwezi, lakini kutokana na dharura ijulikanayo (ugonjwa au kunyonyesha) heidh yake ikasimama. Hukmu yake ni kwamba atakuwa amezuilika kwa muda wa kusubiri usokuwa na kikomo hata kama itakuwa ni muda mrefu. Chini ya hali kama hiyo, itambidi asubiri mpaka damu yake imrudie. Kisha muda wake wa kusubiri utahesabiwa kulingana na masiku itakapobakia damu yake, bila ya jambo lolote jengine. Hatahivyo, ikiwa mwanamke atapata matibabu au atamaliza kunyonyesha, yaani sababu ya kusimama kwa damu itakuwa hakuna, itambidi asubiri kwa mwaka mzima (Eda yake) kuanzia ile tarehe ambayo ametwahirika. Huu ndio msimamo unaokubalika kwa hukmu za ki-fiqh. Mas'ala haya yamefafanuliwa zaidi yakwamba ikiwa sababu ya kukatika kwa damu imeondoshwa, na ikawa damu bado haionekani, basi atakuwa ni kama wale ambao damu zao za heidh zimekatika kutokana na sababu zisizojulikana. Na lau itakuwa hivyo, atasubiri kwa muda wa mwaka mmoja mzima ... yaani, miezi tisa kama muda wa mimba ambao ni wa kutahadhari kwa vile huo ndio muda mkamilifu wa mimba na miezi mitatu ambayo ni miezi ya kusubiri.

Mas'ala: Tuseme Talaka imetolewa baada ya kuithibitisha ndoa, lakini kabla ya kukaa katika faragha na mke na kuingiliana nae, basi hali kama hiyo haihitaji kukaliwa Eda na yule mke. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى) **"Enyi mlioamini! Munapowaowa wanawake waumini, kisha mukawapa talaka kabla hamujaingiliana nao, hawana Eda [muda wa kisheriya wa talaka** (Qur'an 65:4)] **ya kuwahesabia juu yenu. Basi wapeni zawadi, na muwawache huru kwa wema."** (Qur'an 33:49)

Ya Tisa: Fuko La Uzazi Lililo Huru

Fuko la uzazi lisilokuwa na mimba lina uhusiano na hali ya heidh ya mwanamke na pia (lina uhusiano) na matumizi ya baadhi ya Sheriya za ki-Islamu. Kwa mfano, iwapo mwanamke alifiliwa na mumewe na haliyakuwa ni mja mzito, kisha akaolewa na mume mwengine muda mfupi

P. O. Box 85477,
Mombasa,
Kenya.

E-mail: info@qssea.net

QSS (E.A)

جمعية القرآن والسنة في شرق إفرقيا

Tuko katika Tovuti
http://www.qssea.net